

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE

31 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE – TAREHE 31 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa

Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

294. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya katika Jimbo la Lupembe ili kuboresha huduma za afya kwa Wananchi.

295. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa barabara ya Kilomita 3 kwa kuanzia katika Halmashauri ya Geita.

**296. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA
(MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuajiri Watumishi wa kutosha katika Kada za Afya na Elimu nchini.

WIZARA YA MAJI:

**297. ● MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata maji safi na salama.

**298. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatua ndoo kichwani Wanawake wa Mji wa Mlowo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

299. MHESHIMIWA ABEID RAMADHANI IGHONDO (SINGIDA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya Vituo vya Polisi vya Ilongero, Ngamu, Ngimu, Msange na Mtinko Jimbo la Singida Kaskazini.



300. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Igunga.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**301. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, nani anahusika kukamilisha ujenzi wa
Viwanja vya Michezo Nelson Mandela
University ili shughuli za michezo ziendelee.

**302. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kuvuja kwa
Mitihani inayosimamiwa na Vyuo vya Afya
Mwaka 2021.

WIZARA YA NISHATI:

**303. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE
(NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-


Je, ni lini Serikali itaviunganishia umeme Vijiji vya Jimbo la Ndanda vilivyopitiwa na nguzo za umeme wa Msongo wa 33KV kuelekea Masasi.

WIZARA YA KILIMO:


**304. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER
KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inawasaidiaje Wakulima wa Parachichi Iringa ili waweze kulima kilimo chenye tija.



IV. HOJA ZA SERIKALI:



**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA
31 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**